TANGAZO LA SERIKALI NA. 900 la tarehe 15/12/2023

SHERIA YA FEDHA YA SERIKALI ZA MITAA,
(SURA YA 290)

SHERIA NDOGO

*(Imetengenezwa chini ya vifungu vya 7(1) na 16(1))*

# SHERIA NDOGO YA ADA NA USHURU WA MADINI YA UJENZI YA HALMASHAURI YA WILAYA YA KYERWA YA MWAKA 2023

Jina

1. Sheria Ndogo hii itajulikana kama Sheria Ndogo ya Ada na Ushuru wa Madini ya Ujenzi ya Halmashauri ya Wilaya ya Kyerwa ya Mwaka 2023.

Matumizi

2. Sheria Ndogo hii itatumika katika eneo lote la Halmashauri ya Wilaya ya Kyerwa.

Tafsiri

3. Katika Sheria Ndogo hii, isipokuwa kama muktadha utahitaji vinginevyo-

"ada" maana yake ni malipo yatakayolipwa na mtu yeyote kwa Halmashauri kwa ajili ya kupata kibali kinachotolewa na Halmashauri kwa mujibu wa Sheria Ndogo hii;

"Halmashauri" maana yake ni Halmashauri ya Wilaya ya Kyerwa;

"kibali" maana yake ni idhini au ruhusa ya maandishi inayotolewa kwa mujibu wa Sheria Ndogo hii;

"madini ya ujenzi" maana yake ni tarazo, moramu, udongo, kifusi, kokoto, mawe,

mchanga, chokaa na madini mengine yanayotumika katika ujenzi;

"Mkurugenzi" maana yake ni Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Kyerwa na inajumuisha Afisa yeyote atakayeteuliwa kutekeleza majukumu ya Mkurugenzi;

"ushuru" maana yake ni tozo inayotozwa na Halmashauri kwa shughuli zinazohusu ununuzi wa madini ya ujenzi katika eneo la Halmashauri;

"wakala" maana yake mtu, taasisi, kikundi cha watu, kampuni au asasi iliyoteuliwa na Halmashauri kukusanya ushuru wa madini ya ujenzi kwa niaba yake.

Maombi ya kibali

4.-(1) Mtu, taasisi au kampuni inayokusudia kuanzisha machimbo ya madini ya ujenzi katika eneo la Halmashauri itatakiwa kuwasilisha kwa Mkurugenzi maombi ya kibali cha uchimbaji wa madini ya ujenzi kupitia fomu maalumu itakayotolewa na Halmashauri.

(2) Maombi ya kibali yataambatishwa na taarifa zifuatazo:

(a) leseni ya uchimbaji wa madini iliyotolewa na mamlaka husika;
(b) aina ya madini yanayokusudiwa kuchimbwa;
(c) uthibitisho wa umiliki pamoja na ukubwa wa eneo linalokusudiwa kuchimbwa madini ya ujenzi;
(d) mpango wa utunzaji wa mazingira katika eneo la machimbo; na
(e) muhtasari wa mkutano wa kijiji ambacho uchimbaji wa madini ya ujenzi utafanyika ukionyesha kukubaliana na uchimbaji huo.

(3) Ndani ya muda wa siku saba tangu

kupokea maombi, Mkurugenzi atatakiwa kukagua eneo ambalo uchimbaji wa madini ya ujenzi unakusudiwa kufanyika ili kujiridhisha iwapo eneo hilo linafaa kwa shughuli za uchimbaji wa madini ya ujenzi.

(4) Ndani ya muda wa siku saba tangu kukamilika kwa ukaguzi wa eneo linaloombewa kibali, Mkurugenzi atatakiwa kukubali au kukataa maombi hayo na endapo atakataa atatakiwa kutoa sababu za kukataa maombi hayo.

Wajibu wa mpewa kibali

5. Mtu, taasisi au kampuni iliyopewa kibali cha uchimbaji wa madini ya ujenzi itatakiwa:

(a) kuomba kibali kama ilivyoainishwa katika Jedwali la Kwanza la Sheria Ndogo hii;

(b) kulipa ada ya kibali cha uchimbaji wa madini ya ujenzi ya kiasi cha shilingi laki tatu;

(c) kuzingatia masharti ya Sheria Ndogo hii na masharti ya kibali cha uchimbaji wa madini ya ujenzi; na

(d) kulipa ushuru na tozo mbalimbali zitakazotozwa na Halmashauri kwa mujibu wa Sheria Ndogo hii au Sheria Ndogo nyingine iliyotungwa na Halmashauri.

Muda wa uchimbaji na masharti ya usafirishaji

6.-(1) Shughuli za uchimbaji, uuzaji na ununuzi wa madini ya ujenzi katika eneo la Halmashauri zitafanyika kuanzia Saa kumi na mbili kamili asubuhi hadi Saa kumi na mbili jioni ya kila siku.

(2) Bila kujali masharti ya aya ndogo ya (1), Mkurugenzi anaweza kutoa kibali maalumu

kuruhusu shughuli za uchimbaji, uuzaji na ununuzi wa madini ya ujenzi kufanyika nje ya muda ulioainishwa katika aya ndogo ya (1).

(3) Kila mmiliki wa gari linalosafirisha madini ya ujenzi atatakiwa kuhakikisha kuwa gari hilo limefunikwa wakati wote wa usafirishaji wa madini ya ujenzi.

Ushuru wa madini ya ujenzi

7. Kutakuwa na ushuru wa madini ya ujenzi ambao utalipwa na mnunuzi au msafirishaji wa madini ya ujenzi kwa kiwango kilichoainishwa katika Jedwali la Pili la Sheria Ndogo hii.

Vituo vya ukaguzi

8.-(1) Kutakuwa na vituo vya ukaguzi wa malipo ya ushuru wa madini ya ujenzi katika njia zinazoingia au kutoka katika maeneo ya machimbo ya madini ya ujenzi.

(2) Kila dereva wa gari au chombo chochote cha usafiri kilichobeba madini ya ujenzi atatakiwa kusimama katika kituo cha ukaguzi wa malipo ya ushuru wa madini ya ujenzi na kuonesha stakabadhi ya kielektroniki kuthibitisha kulipwa kwa ushuru wa madini ya ujenzi yaliyo katika gari au chombo cha usafiri anachoendesha.

Matumizi ya stakabadhi ya kielektroniki

9. Halmashauri itatakiwa kutoza ada au ushuru kwa kutumia mashine za kielektroniki.

Kufutwa au kusimamishwa kwa kibali

10.-(1) Halmashauri inaweza kufuta au kusimamisha kibali cha uchimbaji wa madini ya ujenzi endapo itajiridhisha kuwa kuna ukiukwaji wa masharti ya Sheria Ndogo hii au masharti ya kibali cha uchimbaji wa madini ya ujenzi.

(2) Kabla ya kufuta au kusimamisha

kibali, Halmashauri itatakiwa kutoa kwa mtu, taasisi au kampuni iliyopewa kibali notisi ya siku saba ya kusudio la kufuta au kusimamisha kibali.

(3) Notisi itakayotolewa kwa mujibu wa aya ndogo ya (2) itaainisha sababu za kufuta au kusimamisha kibali husika.

(4) Endapo kibali kitafutwa au kusimamishwa, mtu, taasisi au kampuni iliyopewa kibali cha uchimbaji wa madini ya ujenzi itakoma kuchimba madini hayo.

Wakala

11. Halmashauri inaweza kuteua mtu, kikundi cha watu, taasisi au kampuni kukusanya ushuru kwa niaba yake.

Makosa na adhabu

12. Mtu yeyote ambaye-

(a) ataanzisha machimbo ya madini ya ujenzi bila kuwa na kibali kilichotolewa chini ya Sheria Ndogo hii;
(b) atasafirisha madini ya ujenzi bila kulipa ushuru;
(c) atachimba madini ya ujenzi kabla au baada ya muda ulioruhusiwa kuchimba;
(d) atasafirisha madini ya ujenzi katika gari ambalo halijafunikwa; au
(e) atamshawishi mtu au kundi la watu kutolipa ushuru,

atakuwa ametenda kosa na akipatikana na hatia atatozwa faini isiyopungua Shilingi laki mbili na isiyozidi Shilingi Milioni moja au kifungo kisichopungua mwaka mmoja na kisichozidi miaka miwili au adhabu zote mbili kwa pamoja yaani faini na kifungo.

Kufifilisha kosa

13. Mkurugenzi anaweza kufifilisha kosa kwa kumtoza mtu yeyote aliyetenda kosa kwa mujibu wa Sheria Ndogo hii kiasi cha Shilingi laki mbili iwapo mkosaji atakiri kosa kwa hiari na kuwa tayari kujaza fomu maalumu iliyoainishwa katika Jedwali la Tatu la Sheria Ndogo hii na kuwa tayari kutimiza wajibu wake kwa mujibu wa Sheria Ndogo hii.

JEDWALI LA KWANZA

*Limetengenezwa chini ya aya ya 5(a))*

KIBALI CHA UCHIMBAJI WA MADINI YA UJENZI

Kibali hiki kimetolewa kwa Bw/Bi ……………………………….……wa SLP………………,KYERWA. Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Kyerwa ameridhia ndugu mtajwa hapo juu, aendeshe shughuli za Kuchimba madini ya Ujenzi katika eneo la ………………………kijiji cha …………………………….kata ya …………………………… baada ya kufanya ukaguzi katika eneo husika ili kutathimini athari za Mazingira.

Kutokana na uzingatiaji wa athari za Mazingira Mchimbaji anaruhusiwa kuchimba madini ya ujenzi katika eneo hilo kwa muda wa miezi kumi na mbili tu. Mwombaji analazimika kuomba tena kibali baada ya muda huo kuisha na ukaguzi utafanyika tena.

TAMKO LA MWOMBAJI;

MIMI……………………………………………………Nipo tayari kufuata masharti ya kibali hiki cha Uchimbaji wa Madini ya Ujenzi ndani ya Halmashauri ya Wilaya ya Kyerwa kwa lengo la kutunza na kuhifadhi mazingira. Nathibitisha kwa hiari yangu nimeelewa vema kibali hiki.

Jina: ……………………………… Saini …………Tarehe …………………

*KWA MATUMIZI YA OFISI;*

Mwombaji amelipia Shilingi
…………………….tarehe…………….mwezi………….mwaka…………..
(Ambatanisha stakabadhi ya malipo na fomu hii)

Jina la Afisa aliyetoa kibali ……………………… Saini ……………
Tarehe ……………….

JEDWALI LA PILI

*(Limetengenezwa chini ya aya ya 7)*

USHURU WA MADINI YA UJENZI

| Na. | Aina ya Madini | Ujazo /Tani | Kiwango cha Ada (Shilingi) |
|---|---|---|---|
| 1. | Mawe | Tani 3 –Tani 7 | 3,000 kwa tripu |
| 2. | Molamu | Tani 3 –Tani 7 | 2,000 kwa tripu |
| 3. | Mchanga | Tani 3 –Tani 7 | 2,000 kwa tripu |
| 4. | Kokoto | Tani 3 –Tani 7 | 5,000 kwa tripu |
| 5. | Mawe, Moramu, Mchanga na Kokoto | Zaidi ya Tani 7 | 3% ya bei ya madini husika |

JEDWALI LA TATU

*(Limetengenezwa chini ya aya ya 13)*

HATI YA KUFIFILISHA KOSA

Mimi;………………………………………………………. nakiri KWA HIARI YANGU MWENYEWE mbele ya;……………………………………..…….ambaye ni Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Kyerwa, kwamba mnamo tarehe;…… ya Mwezi;….…. Mwaka;…….… nilitenda kosa la kukiuka masharti ya aya ya….. ya Sheria Ndogo ya Ada na Ushuru wa Madini ya Ujenzi ya Halmashauri ya Wilaya ya Kyerwa ya Mwaka 2023.

Kwa Mamlaka aliyopewa Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Rorya, niko tayari kulipa kiasi cha Ada au Ushuru ninaodaiwa pamoja na faini.

NATHIBITISHA KWAMBA MAELEZO HAPO JUU NI YA KWELI NA NIMEYATOA MIMI MWENYEWE KWA HIARI YANGU KADRI YA UFAHAMU WANGU:
Leo tarehe:…...... ya Mwezi:………… Mwaka:…………..
Jina:………………………………..…………………….
Saini:…………………………..……………………………
MBELE YANGU :
Jina:………………………….………..……………………
Cheo:…………………………………………………..…….
Saini:…………………………………………………………
Tarehe:……………………………………………………….

Lakiri ya Halmashauri ya Kerywa imegongwa kwenye sheria Ndogo hizi kufutia azimio lililopitishwa katika Mkutano wa Baraza la Madiwani Halmshauri ya Wilaya ya Kyerwa uliofanyika Tarehe …. Mwezi… Mwaka…. na Kushudiwa na Lakiri hiyo ikigongwa mbele ya :-

SACF. JAMES MARCO
*Mkurugenzi Mtendaji*
*Halmashauri ya Wilaya ya Kyerwa*

MH. BAHATI HENERICO
*Mwenyekiti*

*Halmashauri ya Wilaya ya Kyerwa*

NAKUBALI,

Dodoma,
20 Novemba, 2023

MOHAMED OMARI MCHENGERWA (MB)
*Waziri wa Nchi – Ofisi ya Rais,*
*(Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa)*